

Maswali

1. Mbona Farao aliogopa wana wa Israeli?
2. Farao aliweka nani kuwa msimamizi wa Waisraeli?
3. Farao aliambia wakunga wafanye nini?
4. Mamake Musa aliitwa nani?
5. Yokebedi alifanyaje Musa kwa miezi 3?
6. Yokebedi alimtengenezea nini mtoto wake?
7. Yokebedi alificha wapi Safina?
8. Nani alimuokota mtoto?
9. Ni nani alikuwa akiangalia kitakacho fanyika kwa mtoto?
10. Miriamu aliita nani awe wakumulisha mtoto?

Majibu

1. Farao aliogopa wana wa Israeli kwa sababu walikuwa taifa kubwa na lenye nguvu sana.
2. Aliweka wasimamizi kuwachunga Waisraeli.
3. Wakunga waliambiwa kuuwa watoto wavulana.
4. Mamake Musa aliitwa Yokebedi
5. Yokebedi alificha Musa kwa miezi mitatu.
6. Yokebedi alimtengenezea Safina ya unyasi.
7. Yokebedi alificha safina kwenye majani karibu na mto.
8. Binti wa Farao aliokota mtoto.
9. Miriamu alikuwa akiangalia kitakacho fanyika kwa mtoto.
10. Miriamu aliita Yokebedi awe wakulisha mtoto.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

14 Kuzaliwa kwa Musa

Marejeo

Kutoka 2:1 - 10

Kiini cha somo

Kuonyesha ulinzi waajabu wa Mungu kwa watu wake

Maneno maalum

- 1 Farao mgeni (mpya) + Yusufu hakumbukwi + taifa kubwa la nguvu + Farao aogopa + wasimamizi + watumwa
- 2 Wazalishi (wakunga) + watoto wavulana wauwawe + Amramu na Yokebedi + mtoto mvulana afichwa + safina kwa mto + Miriamu achunge
- 3 Binti Farao + mchakazi akachukuwa safina
- 4 Miriamu akamleta Yokebedi + mshahara wa kulea mtoto + Musa + jumba la mfalme

14.1 Kulikuwa na Farao mgeni huko Misri. Hakumkumbuka Yusufu wala vile aliokoa watu wakati wa njaa kubwa.


Wana wa Israeli walikua na wakawa taifa kubwa. Farao mpya akakuwa na uoga. "Wana wa Israeli sasa ni taifa kubwa na wananguvu kuliko sisi," Farao akasema.

Farao akafunya wana wa Israeli watumwa. Waliwawekea wasimamizi ili wafanye kazi ngumu. Walifanya kazi ngumu ya kujengea Farao miji Lakini waliendelea kuwa taifa kubwa zaidi.

14.2 Kwa hivyo Farao akawaambia wakunga wa wana wa Israeli. "Ua wavulana wanaozaliwa na wanawake wa Israeli," Farao alisema.

Kulikuwa na mtu Mwisraeli aliyeitwa Amramu na mkewe Yokebedi, walipata mtoto mvulana aliyekuwa nzuri. Waliogopa kwa maana Farao alitoa amri ya kuwaua watoto wavulana. Walimficha kwa miezi mitatu.

Waliposhindwa kuendelea kumficha, Yokebedi alimtengenezea safina (kikapu) cha unyasi. Alimweka humu na kukiweka ndani ya majani kando ya mto. Yokebedi alimwambia binti wake Miriamu achunge na aangalie ni nini itafanyika kwa mtoto.



14.3 Muda si muda, Binti Farao akaja chini mtoni ili aoge. Alitembea kando ya mto na vijakazi wake. Aliona safina ndani ya majani na akatuma kijakazi wake kukileta. Alipochukuwa hiyo safina, mtoto alianza kulia na akampenda. "Huyu ni mmoja wa watoto wa Waisraeli," alisema.

Miriamu alikuwa akiangalia mda huu wote. Walipompata kakake mtoto, alimkimbilia huyu Binti Farao, "Naweza kwenda kukuletea mlezi kutoka kwa wanawake wa Israeli?" alimuuliza, "Atakulishia motto."

"Enda" Binti Farao alisema.

14.4 Miriamu alimkimbilia mamake Yokebedi, na kumwambia yote yaliyotokea. Miriamu akampeleka Yokebedi mtoni kwa Binti Farao.



"Chukuwa huyu mtoto uende unilishie," Binti Farao alisema, "na nitakulipa mshahara wako." Yokebedi alifurahi sana, akamchukua nyumbani na kumlinda.

"Nitamuita Musa," Binti Farao alisema, "kwa sababu nilimtoa kwa maji."

Yokebedi alimlelea Binti Farao mtoto wake. Alipokuwa mkubwa alimpeleka kwa Jumba la Kifalme na akawa mwana wa Binti Farao.

